# HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

*Mhe. Mwenyekiti na Wajumbe*
*Baraza la Madiwani,*
*Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela.*
***MWANZA***

***YAH: TAARIFA YA MKURUGENZI KATIKA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI KWA ROBO YA PILI (OKTOBA – DISEMBA) TAREHE 13/03/2018 MWAKA WA FEDHA 2017/2018***

## 1.0. UTANGULIZI

***Mhe. Mwenyekiti***, Kwa mujibu wa Kanuni za kudumu za Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela za Mwaka 2014, Mkurugenzi anawajibika kulitaarifu Baraza la Madiwani kwa kutoa taarifa ya matukio mbalimbali ambayo yamefanyika au yanatarajia kutokea katika kipindi cha kila robo ya mwaka.
***Hivyo taarifa hii itagusa maeneo yafuatayo:-***

i. *Taarifa ya Urasimishaji wa makazi holela katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri.*
ii. *Taarifa ya maendeleo ya mradi wa uendelezaji Miji na Majiji (TSCP)*
iii. *Taarifa ya ujio wa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*
iv. *Taarifa ya Maelekezo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika eneo la uwanja wa ndege*
v. *Uboreshaji wa Mindombinu Kituo vya Afya Karume*
vi. *Taarifa ya uingizaji wa taarifa za matumizi ya fedha katika ngazi za vituo vya kutolea huduma za afya, shule za msingi na Sekondari*
vii. *Taarifa za kupokea fedha za kulipa kwa matokeo Sekta ya Elimu (EP4R)*

## 2.0. UFAFANUZI WA TAARIFA

### 2.1. Taarifa ya Urasimishaji wa makazi holela katika maeneo mbalimbali ya halmashauri.

Ili kudhibiti makazi yasiyo rasmi Wilaya inaendelea kutekeleza azma ya Serikali ya kuboresha makazi kwa kufanya upimaji shirikishi ambapo katika zoezi la kurasimisha makazi ambapo jumla ya Hati 5,277 kati ya Hati 16,141 zimeandaliwa katika maeneo yaliyorasimishwa. Pia jumla ya viwanja 15,890 kati ya viwanja 16,141 ambayo ni sawa na asilimia 98.44 vimepimwa na kupata usajili kwa Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani.

Pamoja na mafanikio tajwa hapo juu, kumekuwepo na changamoto katika utekelezaji wa zoezi hili ambazo ni;

1. Mwitikio mdogo wa wananchi katika kuchangia gharama za kuandaliwa Hati milki.
2. Wananchi kutokuwasilisha nyaraka muhimu za kukamilisha Hati milki kama Uthibitisho wa Uraia, picha n.k.
3. Migogoro iliyotokana na Wananchi kutokuwa tayari kuachia maeneo ya huduma za jamii, kama vile, barabara, masoko, maeneo ya wazi n.k. hivyo kuchelewesha ukamilishaji wa Ramani za Upimaji na Umilikishaji.
4. Wananchi kuvamia maeneo yaliyotengwa na kupimwa kwa shughuli za huduma za jamii kama vile Zahanati, maeneo ya wazi na kutokuwa tayari kuchangia upatikanaji wa maeneo mbadala ya huduma hizo muhimu.

Pamoja na changamoto zilizojitokeza, Halmashauri imekuwa ikizikabili kwa njia mbalimbali ambazo ni pamoja na;-

- Kufanya mikutano ya kuhimiza wananchi kulipia gharama za Upimaji na Umilikishaji katika Kata zinazohusika. Waheshimiwa Madiwani na Mhe Mbunge wa Jimbo la Ilemela walishiriki kikamilifu katika mikutano hiyo. Aidha, matangazo kwa kutumia gari la matangazo, Pembe kwenye

Mitaa husika na vyombo vya habari vya Radio na Televisheni yamefanyika.

- Vikao vya uelimishaji kwa wananchi vikihusisha viongozi wa Mitaa na Kamati za Urasimishaji ili kuachia maeneo hayo ya huduma muhimu vilifanyika.

Pia Halmashauri imeendelea na kuboresha mfumo wa upatikanaji wa takwimu za viwanja. Katika kutekeleza suala hili jumla ya viwanja 35,336 tayari vimeingizwa katika mfumo ambapo lengo kwa mwaka huu ni kufikia viwanja 40,000 kuingizwa katika mfumo

## 2.2. Taarifa ya Maendeleo ya Mradi wa TSCP

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, ili kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa 2015, Halmashauri ya Manispaa katika mwaka wa Fedha 2017/2018, ilipanga kujenga barabara ya lami kutoka Buswelu – Kiseke – sabasaba yenye urefu wa kilomita 9.7. Nipende kulijulisha Baraza hili kuwa, kazi ya ujenzi itaanza mwezi Mei 2018 badala ya mwezi Machi kama ilivyotolewa taarifa katika Baraza la Madiwani lililopita kwani mpaka sasa taratibu za zabuni zimekamilika. Barabara hii inafadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Tanzania, Benki ya Dunia kupitia mradi wa uendelezaji miji na Majiji (TSCP) kwa kushirikiana na Halmshauri ya Manispaa ya Ilemela.

Wakati huohuo, Jumla ya wananchi 22 Wamelipwa fidia na fedha kiasi cha **Tshs 306,008,000/= kimetumika kati ya Tshs 636,626,000.00 zilizotengwa.** Aidha, zoezi la uhakiki na ulipaji Fidia bado linaendelea na baadhi ya waliolipwa wamevunja nyumba zao ikiwa ni pamoja na kukata miti ili kuacha wazi eneo la mradi.

Napenda kut oa wito kwa waheshimiwa Madiwani na wananchi kwa ujumla kushirikiana wakati wa utekelezaji wa mradi huu pindi utakapoanza kutekelezwa ili kusiwe na mkwamo utakaotokana na malalamiko yasiyokuwa ya msingi.

### 2.3 Taarifa ya Ziara ya Mhe. Waziri Mkuu Katika Wilaya ya Ilemela

Mnamo tarehe 20/02/2017, Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kassimu Majaliwa Majaliwa alifanya ziara katika Wilaya za Mkoa wa Mwanza ambapo Wilaya yetu alitembea tarehe 20/02/2018.

Pamoja na mambo mengine, Mhe. Waziri Mkuu alifanya shughuli zifuatazo;

(i) Kuongea na waheshimiwa Madiwani na Watumishi wa Serikali ambapo alisisitiza uwajibikaji wa watumishi katika kuwatumikia wananchi kwa uadilifu;

(ii) Pia aliweza kutembelea mradi wa kiwanda cha Mwanza Plastic ambapo alizindua kiwanda hicho;

(iii) Kutembelea kituo cha Afya karume ambapo aliweka jiwe la msingi la ukarabati wa kituo hicho. Mhe waziri Mkuu aliipongeza Halmashauri kwa kutekeleza vema na kwa uadilifu mkubwa mradi huo; na

(iv) Kufanya mkutano wa hadhara katika katika shule ya msingi Bugogwa ambapo aliiangiza Halmashauri kushughulikia mgogoro wa ardhi katika Kata ya Shibula.

### 2.4 Taarifa ya Maelekezo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika eneo la uwanja wa ndege.

Mnamo tarehe 24/03/2018 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt John Pombe Joseph Magufuli alipita katika uwanja wa ndege wa Mwanza wakati akitokea nchini Uganda na akielekea Chato. Akiwa katika uwanja wa ndege Mhe. Rais

alipata wasaa wa kuongea na Watumishi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege pamoja na Taasisi waliokuwepo hapo na alitoa maagizo kuwa Taasisi za Uwanja wa ndege na Jeshi la wananchi Tanzania zibainishe eneo linalohitaji kwa ajili ya uwanja wa ndege na kama kuna eneo ambalo halihitajiki wananchi wamilikishwe.

Aidha, mpaka sasa Halmashauri kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Wizara ya Ulinzi, Wizara ya Ardhi na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege wameanza kushughulikia suala hilo na hatua inayoendelea ni kubainisha ukubwa wa eneo la uwanja wa ndege na jeshi linalohitajika kwa ajili matumizi ya Taasisi hizo.

### *2.5 Taarifa ya uboreshaji wa kituo cha Afya Karume*

Serikali ilitoa kiasi cha **Tshs 500,000,000** kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya kituo cha Afya Karume kilichoko kata ya Bugogwa. Utekelezaji wa ujenzi hdi kuishia Disemba 2017, tayari **umekamilika 99 na kiasi cha Tshs 488,032,623.93** kutoka Serikali Kuu zilikuwa zimetumika kwa kujenga majengo yafuatayo;

i. Jengo la Upasuaji
ii. Jengo la kujifungulia wajawazito
iii. Nyumba ya Mtumishi
iv. Jengo la maabara
v. Jengo la Kuhifadhia maiti

Aidha, katika ujenzi huu, Wilaya imetekeleza maelekezo ya Serikali ya awamu ya tano kwa kumia vema fedha hizi mradi. Katika kutekeleza mradi huu wilaya imetekeleza kwa kutumia mfumo wa "***Force account".*** Faida iliyopatikana kwa wilaya kutekeleza bila kutumia mkandarasi ni kuwa, imewezesha kuokoa fedha za Umma zaidi ya Tshs 139,000,000.

Pia, Serikali imeidhinisha kiasi cha **Tshs. 220,000,000/=** ikiwa ni gharama za ununuzi wa vifaa tiba, vifaa vya hospitali na

vitendanishi kwa ajili ya kituo cha Afya karume. Fedha hizo zimepelekwa moja kwa moja MSD ambaye ndiye analeta vifaa hivyo. Hadi sasa kituo kimepokea vifaa vyenye thamani ya **Tshs. 48,981,300** ambavyo baadhi vimeingia kwenye majengo yaliyokamilika na vingine vinangojea ukamilishaji wa majengo.

### 2.6 Taarifa ya uingizaji wa taarifa za matumizi ya fedha katika ngazi za vituo vya kutolea huduma za afya, shule za msingi na Sekondari

Kulingana na melekezo ya Serikali ya mfumo wa uandaaji wa taarifa za mapato na matumizi kwa fedha zinazopelekwa ngazi za chini yaani vituo vya kutolea huduma za Afya, Shule za Msingi na Sekondari (FFAS), Napenda kulifahamisha Baraza hili kuwa, katika kipindi cha kuanzi Oktoba 2017 – Disemba 2017 yaani robo ya pili, Halmashauri imekuwa ya kwanza Kimkoa na kuandikiwa barua ya kupongezwa kwa kufanya vizuri katika zoezi hili. Tunawapongeza wataalamu wote walioshiriki katika zoezi hili.

### 2.7 Taarifa za kupokea fedha za kulipa kwa matokeo Sekta ya Elimu (EP4R)

Kutokana na Halmashauri kuzingatia masharti na vigezo vilivyowekwa na Serikari ya fedha za malipo kwa matokeo, tumefanikiwa kuongeza mgao wa fedha kutoka Tshs 81,000,000 mwaka huu 2016/2017 hadi Tshs 313,000,000 Mwaka 2017/2018 sawa na ongezeko la **Tshs 232,000,000.** Pamoja na ongezeko hili, bado tunatakiwa tuongeze bidi na endepo Halmashauri itaongeza umakini katika uzingatiwaji wa vigezo, tunatarajia kupata mgao zaidi ya Tshs 700,000,000

Naomba kuwasilisha

John Paul Wanga
Mkurugenzi wa Manispaa
**ILEMELA**